# JARIDA LA USHIRIKA

ISSN 2714 - 2175 Toleo Na: 006 Aprili - Juni, 2021




## USHIRIKA AFYA KUONGEZA KASI YA MAENDELEO KATIKA USHIRIKA







*"Ushirika - Pamoja Tujenge Uchumi Imara na Endelevu"*

# YALIYOMO


| | |
|---|---|
| USHIRIKA AFYA KUMWEZESHA MKULIMA KUWA NA UHAKIKA WA MATIBABU | 03 |
| CRDB NA NHIF ZAINGIA MKATABA WA MAKUBALIANO KUBORESHA "USHIRIKA AFYA" | 04 |
| NMB, NHIF KUWAWEZESHA WAKULIMA WALIOKO NDANI YA USHIRIKA KUJIUNGA NA BIMA YA AFYA | 06 |
| WANAUSHIRIKA CHAGUENI VIONGOZI BORA – WAZIRI MKENDA | 08 |
| WAKULIMA WA TUMBAKU KUPATA NEEMA KUPITIA USHIRIKA - MHE. BASHE | 09 |
| USHIRIKA KUJA NA SULUHISHO YA VIFUNGASHIO | 11 |
| VIONGOZI WA USHIRIKA IRINGA WAHIMIZWA KUSIMAMIA STAKABADHI YA GHALA | 13 |
| NAIBU MRAJIS AHIMIZA UADILIFU KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA | 15 |
| WAKULIMA WA MVOMERO WAANZA KUNUFAIKA NA ONGEZEKO LA BEI YA KOKOA KUPITIA MFUMO WA STAKABADHI ZA GHALA | 16 |
| STAKABADHI ZA GHALA KUENDELEA KUMPAISHA MKULIMA | 18 |
| HALI YA UKUSANYAJI NA UUZAJI WA MAZAO YA KOROSHO NA UFUTA MKOANI LINDI KWA MSIMU 2020/2021 | 20 |
| USHIRIKA KUJALI JAMII KWA VITENDO | 22 |
| MCHANGO WA VYAMA VYA USHIRIKA WA NYUMBA KUFIKIA AZMA YA NYUMBA KWA WOTE NA UKUAJI WA MIJI | 24 |
| USHIRIKA WA NYUMBA NA MALENGO YA MAENDELEO ENDELEVU | 24 |
| UMUHIMU WA VYAMA VYA USHIRIKA WA NYUMBA KATIKA MNYORORO WA THAMANI WA NYUMBA | 25 |

# USHIRIKA AFYA KUMWEZESHA MKULIMA KUWA NA UHAKIKA WA MATIBABU

- **Tumekusudia Kuimarisha Usimamizi wa Ushirika**



*Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Dkt. Benson Ndiege*

Kwanza kabisa napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia nafasi nyingine ya kuendelea na majukumu ya kujenga Taifa. Nichukue fursa hii kutoa pole kwa wote kutokana na kuguswa kwa namna moja au nyingine na marathi ya COVID-19 ambayo yameathiri wengi katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Kama mnavyofahamu kuwa afya ni msingi wa maendeleo ya mtu na Taifa kwa ujumla, kutokana na umuhimu wa suala hilo Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa kushirikiana na NHIF, CRDB na NMB inaunga mkono juhudi za Serikali katika azma ya kupanua wigo wa huduma za afya kwa wakulima kupitia huduma ya "***Ushirika Afya***".

Ushirika afya ni huduma ambayo mabenki yenye mkataba na Shirika la Taifa la Bima ya Afya (NHIF) yatakuwa yakisaidia kulipa gharama za bima ya afya (premium) na wakulima kulipaZada ya kuuza mazao yao. Mpango huu unatoa fursa kwa mkulima kusajiliwa katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kupitia chama chake cha msingi cha ushirika wa mazao ambapo Mwanachama wa *Ushirika Afya* atachangia Shilingi 76,800 kwa mwaka na atapatiwa kadi ya matibabu ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ambayo ataitumia kupata matibabu katika vituo zaidi ya 6,000 vilivyosajiliwa na Mfuko nchi nzima.

Ni kutokana na manufaa anayoyapata Mwanachama wa NHIF katika utaratibu wa *Ushirika Afya* ninazipongeza benki zote zilizojitokeza kutoa mkopo usiokuwa na riba kwa mkulima mwanaushirika kumwezesha kujiunga na kufaidika na mafao yanayotolewa na Mfuko huu.

Aidha, kupitia utaratibu huu mkulima ana fursa ya kumwandikisha mwenza wake, mzazi au mzazi wa mweza kwa kuongeza malipo ya TZS 76,800 kwa kila mmoja kwa mwaka. Endapo mwanachama wa Ushirika Afya atahitaji kuwasajili watoto katika mpango huu atalipa TZS 50,400 kwa mwaka kwa kila mtoto chini ya miaka 18.

Mwanachama wa NHIF katika utaratibu wa Ushirika Afya apata mafao yote yanayotolewa na Mfuko sawa sawa na wanachama wengine chini ya Mfuko huu wanaojiunga kwa taratibu nyingine. Mafao hayo yanahusisha gharama za: Kujiandikisha na Kumwona daktari; Dawa zote muhimu zilizoidhinishwa na Serikali; Vipimo vidogo na vikubwa; Kulazwa; Upasuaji mdogo, mkubwa pamoja na upasuaji wa kujifungua kwa wanawake; Matibabu ya kinywa na meno; Matibabu ya macho pamoja na miwani ya kusomea; Mazoezi ya kimatibabu ya viungo (physiotherapy); Vifaa saidizi kama magongo, vishikizi vya shingo

Vilevile mwanachama atatumia kadi yake katika vituo zaidi ya 6,000 nchi nzima kuanzia zahanati hadi Hospitali za rufaa za serikali, binafsi na hata za madhehebu ya dini Pamoja na maduka ya dawa yaliyosajiliwa na NHIF.

# CRDB NA NHIF ZAINGIA MKATABA WA MAKUBALIANO KUBORESHA "USHIRIKA AFYA"

**Benki ya CRDB imesaini mkataba wa makubaliano na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kurahisisha upatikanaji wa bima ya afya kwa wakulima ambapo ushirikiano huo utawawezesha wakulima kupata bima ya afya za NHIF kwa mkopo. Huduma hiyo ambayo imepewa jina la "Ushirika Afya Premium Loan" itatolewa kwa wakulima ambao wapo katika Vyama vya Ushirika huku pia ikiwanufaisha wategemezi wao, kwa maaana ya mke/ mume na watoto.**




*Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya Benard Konga (kushoto) akikabidhiana mikataba ya huduma za Ushirika na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB Abdulmajid Nsekela (kulia), Mrajis wa Vyama vya Ushirika Dkt. Benson Ndiege (katikati) akishuhudia makabidhiano hayo, Dar es Salaam*

Hafla ya utiajisaini mkataba wa huo wa makubaliano imefanyika jijini Dar es Salaam tarehe 05 Mei, 2021 kati ya Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela na Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Bw. Bernard Konga; na kushuhudiwa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndiege.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela amesema katika makubaliano hayo Benki ya CRDB itakuwa ikisaidia kulipa gharama za bima ya afya (premium) na wakulima kulipa mwisho wa msimu baada ya kuuza mazao yao.

"Mkopo hutolewa kulingana na kiwango cha gharama za malipo ya bima ya afya (premium) ambapo kwa mtu mzima ni shilingi 76,800 na mtoto shilingi 50,400," aliongezea Nsekela huku akibainisha kuwa mkopo huo wa bima ya afya utatolewa bure bila ya makato wala riba yoyote.

Kupitia huduma hiyo ya "Ushirika Afya Premium Loan", Mkulima pia anaweza kuchukua kifurushi cha familia cha malipo ya shilingi 355,200 ambapo atapata bima ya afya kwa watu 6 (watu wazima 2, watoto 4). Kifurushi hiki kimeanzishwa ili kuhamasisha wakulima kukata bima kwa familia zao.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Bernard Konga, amesema kuwa, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya umejipanga kuhakikisha unawahudumia kikamilifu wakulima ili wawe na uhakika na shughuli zao za kilimo katika kipindi chote cha mwaka.

"Lengo kubwa la mpango huu ni kuwawezesha wakulima wawe na uhakika wa afya zao kwa maana ya kupata huduma za matibabu wakati wowote wanapozihitaji na kwa upande wa Mfuko tumeboresha zaidi huduma zetu ili mwanachama wetu asipate usumbufu wa aina yoyote," amesema Konga.

Akizungumza kwenye uzinduzi wa mpango huu, Mrajis wa Vyama vya ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndiege amezipongeza CRDB na NHIF kwa kuwajali wakulima na kuwapatia uhakika wa matibabu wakati wote kupitia "Ushirika Afya Premium Loan".

"TCDC ipo tayari kushirikiana na Wadau wenye nia njema ya kuendeleza Wanaushirika katika nyanja mbalimbali za maendeleo ikiwemo afya na nyinginezo. Tutashirikiana na yeyote mwenye dhamira ya kweli kumnufaisha Mwanaushirika na hatutasita kuchukua hatua kwa yeyoye atakayekwenda kinyume na Sheria au taratibu zilizowekwa," amesema Dkt. Ndiege.



*Watendaji mbalimbali wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) pamoja na Benki ya CRDB wakiwa katika hafla ya makabidhiano ya mikataba kati ya NHIF na Benki ya CRDB Mkoani, Dar es salaam*




*Afisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa NMB, Filbert Mponzi (kushoto) Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya Benard Konga (kulia) baada ya utiaji saini wa mkataba wa huduma ya Ushirika Afya, katikati ni Naibu Mrajis wa Vyama vya Ushirika Collins Nyakunga*

# NMB, NHIF KUWAWEZESHA WAKULIMA WALIOKO NDANI YA USHIRIKA KUJIUNGA NA BIMA YA AFYA

Benki ya NMB na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) wameingia makubaliano rasmi ya kuwawezesha wakulima walioko ndani ya vyama vya ushirika nchini kunufaika na huduma za matibabu kupitia mpango wa bima ya afya kwa wakulima unaojulikana kama Ushirika Afya.

Katika makubaliano haya, Benki ya NMB itamlipia mkulima gharama za bima ya afya kwa wakati na mkulima huyu atarejesha mkopo huo bila riba wakati wa msimu wa mavuno na baada ya mauzo ya mazao husika.

Akizungumza katika uzinduzi wa mpango huo, Afisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa NMB, Filbert Mponzi, alisema lengo lao ni kuwafikia wakulima zaidi 300,000 ndani ya kipindi cha miaka mitatu. Alisema wanufaika wa mpango huu ni pamoja na wateja na wasiyo wateja wa benki hiyo, lakini mwanzoni walengwa ni wakulima wa pamba, korosho, kahawa, katani na mahindi kote nchini.

Bwana Mponzi alisema makubaliano hayo ni mojawapo ya nia ya NMB kuunga mkono juhudi za Serikali katika kuhakikisha



*Afisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa NMB, Filbert Mponzi (kushoto) Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya Benard Konga (kulia) wakionesha mkataba wa huduma ya Ushirika Afya, katikati ni Naibu Mrajis wa Vyama vya Ushirika Collins Nyakunga*

Watanzania wengi wanakuwa na bima ya afya. Hata hivyo, kwa kutambua tamaduni mbalimbali za Kitanzania, malipo ya huduma hiyo yatazingatia ukubwa wa familia kama ifuatavyo: Mkulima mwenyewe TZS 76,800 kwa mwaka; Bima ya mtoto TZS 50,400 kwa kila mtoto kwa mwaka; Familia ya mkulima, mwenza wake na watoto wawili TZS 254,400 kwa mwaka; na Familia ya mkulima, mwenza wake na watoto wanne TZS 355,200 kwa mwaka.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Bw. Bernard Konga, alisema kuwa, ushirikiano huu na Benki ya NMB utamwezesha mkulima na familia yake kupata huduma zote za matibabu katika mtandao mpana wa vituo zaidi ya 6,000 Tanzania Bara na Zanzibar kuanzia ngazi ya Zahanati hadi Hospitali ya Rufaa ya Taifa.

Mgeni rasmi katika tukio hilo, Naibu Mrajis wa Vyama vya Ushirika, Udhibiti na Usimamizi wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Bw. Collins Nyakunga, alizipongeza Benki ya NMB na NHIF kwa jitihada za kuhakikisha wakulima wanapata bima ya afya na hawatatumia tena pesa taslimu kujitibia. Aliwaasa wakulima kote chini kuchangamkia fursa hii kwani ni nafuu.




*Picha ya Pamoja ya watendaji wa Benki ya NMB, Mfuko wa Taifa wa Bima ya afya (NHIF) pamoja na Naibu Mrajis wa Vyama vya Ushirika (katikati) Collins Nyakunga wakati wa hafla ya utiaji saini wa mktaba wa Ushirika Afya*

# WANAUSHIRIKA CHAGUENI VIONGOZI BORA – WAZIRI MKENDA




*Waziri wa Kilimo, Mhe Prof. Adolf Mkenda, akizungumza kwenye mkutano mkuu wa 36 wa Chama Kikuu cha Ushirika Mkoani Kilimanjaro (KNCU)*

Waziri wa Kilimo, Mhe Prof. Adolf Mkenda, amewataka wanachama wa Vyama vya Ushirika kusimama imara wakati wa uchaguzi katika kuhakikisha wanapatikana viongozi bora ambao wataviwezesha vyama vya ushirika

Waziri Prof. Mkenda ameyasema hayo tarehe 28 Juni, 2021 wakati akizungumza kwenye mkutano mkuu wa 36 wa Chama Kikuu cha Ushirika Mkoani Kilimanjaro (KNCU) ambapo amesisitiza kuwa serikali inahitaji sheria hiyo ifanyiwe marekebisho ili kuiwezesha kuleta tija kwenye ushirika.

Amesema kuwa Serikali ipo katika mchakato wa kufanya marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2013 lengo likiwa ni kuondoa madhaifu yanayodidimiza Vyama nchini. Aidha, Waziri Mkenda amewataka wanaushirika kuipitia Sheria hiyo na kutoa maoni ambayo yatawezesha kuiboresha na kuifanya kuwa na tija katika Vyama vya ushirika nchini.

"Ingekuwa ni mamlaka yangu ningesema viongozi wote wa Bodi waondoke na wasigombee na tuchague wengine, ila kwasababu Ushirika ni mali ya wanaushirika niwaombe mtumie nafasi yenu kuhakikisha mnawashawishi wale wenye uwezo kugombea nafasi za uongozi," amesema Waziri Mkenda.

Akizungumza katika mkutano huo, Mrajisi wa wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndiege, amesema mkutano Mkuu wa uchaguzi wa KNCU uliahirishwa kwa lengo la kutoa fursa kwa wanachama kuchagua viongozi bora ambao watakuwa na uwezo na ubunifu.

*Mrajisi wa wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndiege, akizungumza kwenye mkutano mkuu wa 36 wa Chama Kikuu cha Ushirika Mkoani Kilimanjaro (KNCU).*



# WAKULIMA WA TUMBAKU KUPATA NEEMA KUPITIA USHIRIKA - MHE. BASHE

Mradi wa Pamoja wa Wakulima wa zao la Tumbaku Tobacco Cooperative Joint Enterprise Limited (T.C.J.E) wametakiwa kutumia Mfumo wa Ununuzi wa Pamoja Bulk Procurement (B.P.S) kwa lengo la kusaidia wakulima wa Tumbaku kupitia Vyama vya Ushirika kupata pembejeo za kilimo kwa bei nafuu.

Maagizo hayo yametolewa na Naibu Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein Bashe Aprili 2021 wakati akifungua rasmi Mkutano Mkuu wa 3 wa T.C.J.E Mkoani Morogoro. Aidha, Naibu Waziri ameeleza kuwa ili mkulima wa Tumbaku aweze kupata pembejeo ikiwemo Mbolea kwa gharama nafuu ni vyema Mradi huo ukafanya taratibu za kukusanya mahitaji ya pembejeo za wakulima wa Tumbaku kutoka kwenye Vyama vya Ushirika wanachama wa Mradi huo. Akiongeza kuwa kufanya hivyo kutapunguza riba za gharama za mikopo ya mabenki, mianya ya ubadhilifu na kuondokana na madeni hewa ambayo yamekuwa yakijitokeza mara kwa mara.

"T.C.J.E katika msimu mpya wa Tumbaku mwaka huu 2021 hakikisheni mahitaji ya wakulima ya Mbolea yanakusanywa mapema na mnunuzi anasambaza mbolea hiyo moja kwa moja kwa wakulima kupitia Vyama vya Ushirika," alisema Naibu Waziri

Mhe. Bashe alieleza kuwa Kilimo ni Sekta muhimu inayochangia kutoa ajira kwa watanzania kwa wastani wa asilimia 60 hadi 75 na kuchangia pato la Taifa kwa wastani wa asilimia 25. Hata hivyo, Naibu Waziri amebainisha kuwa mapato kutokana na zao la Tumbaku kwa sasa yameshuka kutoka



*Naibu Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein Bashe akiongea na wajumbe wa mkutano wa 3 wa Mradi wa Pamoja wa Wakulima wa zao la Tumbaku Tobacco Cooperative Joint Enterprise Limited (T.C.J.E)*

Dola Millioni 300 hadi 146.5 jambo ambalo linachangiwa na kushuka kwa uzalishaji pamoja na kupungua kwa matumizi ya zao hilo.

Pamoja na mambo mengine Naibu Waziri amesema bado Serikali ina dhamira ya

kuendelea kulinda na kusimamia zao la Tumbaku. Akiongeza kuwa Ilani ya Chama Tawala imetoa maelekezo mahususi ya kuimarisha na kujenga Ushirika.

Ili kuhakikisha kuwa Ushirika unaendelea kuendeshwa kwa kufuata Sheria Naibu Waziri Bashe amemuagiza Mrajis wa Vyama vya Ushirika kukamilisha ripoti ya baadhi ya Vyama vya Ushirika ambavyo vina shutuma za ubadhilifu na ripoti hizo ziwasilishwe katika Mamlaka husika kwaajili ya hatua zaidi.

Akiongea wakati wa Mkutano huo Naibu Waziri amempongeza Mrajis na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Dkt. Benson Ndiege kwa utekelezaji wa kuanza utaratibu wa kutumia wahitimu wa Vyuo vikuu katika shughuli za uendeshaji wa Vyama vya Ushirika kwa lengo la kutoa fursa kwa wahitimu hao kujitolea kutumia weledi wao katika nyanja mbalimbali na wao kupata uzoefu wa kazi. Alisema kuwa hatua hiyo ni jambo la kupongezwa kwani wahitimu wengi wanamaliza vyuo na hawana sehemu za kukuza taaluma zao na wakati huohuo Ushirika unapata fursa ya watendaji wasomi watakaoongeza tija kwenye vyama hivyo.

Mkutano huo ulifuatiwa na Uchaguzi wa Viongozi wa T.C.J.E uliowezesha kupata Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti pamoja na Wajumbe wa Bodi uliofanyika kwa mujibu wa Sheria Na.6 ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2013. Hatua ambayo itafuatiwa na Mafunzo elekezi, makabidhiano, fomu za kiapo na maadili yatakayowezesha kuzingatiwa kwa Sheria, Kanuni na Taratibu za Ushirika.



*wajumbe wa mkutano wa 3 wa Mradi wa Pamoja wa Wakulima wa zao la Tumbaku Tobacco Cooperative Joint Enterprise Limited (T.C.J.E) wakifuatilia hotuba na maelezo yaliyokuwa yakitolewa na Naibu Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein Bashe, Mkoani Morogoro*

# USHIRIKA KUJA NA SULUHISHO YA VIFUNGASHIO

Chama Kikuu cha Ushirika Songea Namtumbo (SONAMCU LTD) Ruvuma kimesema tayari chama hicho kiko katika ujenzi wa Kiwanda cha vifungashio kwa lengo la kuhakikisha wakulima Mkoani Ruvuma wanaondokana na changamoto ya Vifungashio vya mazao ya mahindi, ufuta, soya na mbaazi.

Hayo yamesemwa na Meneja wa SONAMCU Juma Mwanga wakati akitoa maelezo kwa Mrajis wa Vyama vya Ushirika Dkt. Benson Ndiege alipotembelea kuona maendeleo ya mradi huo uliopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo Mkoani Ruvuma.

Akitoa maelezo ya mradi Meneja Juma Mwanga ameeleza kuwa licha ya Kiwanda hicho kuzalisha vifungashio kwa bei nafuu na upatikanaji rahisi wa vifungashio kwa wakazi wa Ruvuma na kuongeza mapato kwa wananchi mkoani hapo. Alisema Kiwanda hicho kinamilikiwa na wanachama wa SONAMCU kwa asilimia 100 na kinatarajia kugharimu Shillingi 3, 983,889, 800 za kitanzania. Akibainisha kuwa mradi huo ulianza mwaka 2020 na kukadiriwa kukamilika ifikapo 2022.

"Kwa sasa SONAMCU inapata bidhaa ya vifungashio kutoka Dar es salaam lakini



*Wafanyakazi wakiwa katika hatua mbalimbali za ujenzi wa Kiwanda cha Vifungashio kinachojengwa na Chama Kikuu cha Ushirika cha (SONAMCU LTD) Mkoani Ruvuma*



*Muonekano wa Jengo la Kiwanda cha kutengeneza vifungashio kinachojengwa na Chama Kikuu cha Ushirika cha (SONAMCU LTD) Mkoani Ruvuma*

tunatarajia kiwanda kitakapokamilika kitakuwa na uwezo wa kuzalisha vifungashio Millioni 10 kwa mwaka," alisema Meneja

Aidha, Meneja alieleza kuwa hadi kufikia hatua hiyo ya ujenzi kiwanda hicho kinajengwa kwa kutumia mapato ya ndani kwa asilimia (100%) mapato ambayo yanatokana na vyanzo mbalimbali vya Chama hicho.

Katibu Tawala Wilaya ya Namtumbo Aden Nchimbi katika ziara hiyo amesema Wilaya ya Namtumbo inatarajia kunufaika na mradi huo kutokana na ajira zitakazozalishwa na kiwanda hicho na kuchochea maendeleo ya Wananchi wa eneo hilo pamoja na Mkoa wa Ruvuma.

Kwa upande wake Mrajis Dkt. Ndiege amepongeza ujenzi wa Kiwanda hiko akibainisha kuwa soko la vifungashio hivyo ni kubwa kutokana na mazao mbalimbali yanayozalishwa na Vyama vya Ushirika ndani na nje ya Mkoa wa Ruvuma.

"Kutokana na uhitaji mkubwa wa vifungashio vya mazao ni matarajio yetu kuwa Vyama vya Ushirika vitakuwa wateja na wanunuzi wakubwa wa vifungashio hivyo na nipongeze Chama hiki kwa kuendelea kuunga mkono juhudi za Serikali za kuendeleza Viwanda nchini," alisema Dkt. Ndiege

# VIONGOZI WA USHIRIKA IRINGA WAHIMIZWA KUSIMAMIA STAKABADHI YA GHALA

**Viongozi wa Vyama vya Ushirika wamepewa wito kusimamia matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala ili kuhakikisha wakulima wanapata masoko ya mazao yao na bei zenye tija kwa kuweka vipaumbele vya mipango ya ujenzi wa maghala kuanzia ngazi ya vijiji.**

Wito huo umetolewa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Iringa kupitia hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Katibu tawala Msaidizi Uchumi Elias Luvanda wakati akifungua Mkutano Mkuu wa 20 wa mwaka wa wanachama wa Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Iringa IFCU (1993) Ltd, uliofanyika Mei 07, 2021 Mkoani Iringa.

Katibu Tawala Msaidizi Luvanda amesema Serikali inahamasisha na kuendeleza wakulima kwa kuhakikisha Mfumo wa Stakabadhi ya Ghala unaimarika. Hivyo, amewataka Viongozi katika mkutano huo kuweka mipango yenye malengo ya kuongeza maghala ya kuhifadhi mazao ya wakulima ili kukabiliana na changamoto ya uchache wa maghala na kuzingatia matumizi bora ya maghala.

Aidha, amewataka viongozi wa Ushirika kuwa wasimamizi wazuri wa rasilimali za Vyama vya Ushirika, kuwajibika kwa wanachama wao kwa kufuata misingi na taratibu za Ushirika zitakazosaidia kuondokana na matumizi mabaya ya mali za wanachama pamoja na ubadhilifu.

Mrajis wa Vyama vya Ushirika Dkt. Benson Ndiege akiongea kwa niaba ya wanaushirika amesema Vyama vya Ushirika vitaendelea kutoa ushirikiano na kuvitaka Vyama vya Ushirika kuanzia ngazi ya Vyama vya msingi kutimiza wajibu wao wa Kiushirika kama vile kuandaa makisio, kufanya mikutano mikuu ya mwaka pamoja na kuhakikisha wanachama wanalipa hisa za chama. Hivyo, kuwezesha Chama kikuu kufanya kazi vizuri na hatimaye mfumo wote wa Ushirika kutimiza wajibu wake.

**"Wanachama wa Ushirika ndio wamiliki wa Vyama vya Ushirika, hivyo viongozi wa Ushirika mnawajibika kwa wanachama wenu kuhakikisha mnatoa taarifa za utendaji, taarifa za fedha na maendeleo ya Vyama kupitia mikutano pamoja na matakwa mengine ya Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013," alisema Mrajis**

Aidha amewataka wajumbe wa Mkutano kusoma taarifa zinazotolewa na kuhoji pale inapobidi kuhusu masuala ya uendeshaji wa Chama chao kwani Mkutano Mkuu ndio ngazi ya juu ya maamuzi ya Chama

Hakikisheni mnafuatilia taarifa zitakazoendelea katika Mkutano huu pale mnapoona hamridhiki mna haki ya kuhoji, kupata majibu pamoja na kupitisha makisio na baada ya hapo Mrajis Msaidizi wa Mkoa na Maafisa Ushirika wanaidhinisha kwa mujibu wa Sheria.

Mrajis amewataka Viongozi wa Vyama vya Ushirika kuwa wabunifu kwa kubuni miradi mbalimbali yenye tija na maendeleo kwa Vyama vyao. Akiongeza kuwa ni muhimu Wanachama wa Ushirika waweze kupata thamani ya kujivunia vyama vyao kupitia huduma za Vyama zitakazowatofautisha wanachama na wasio wanachama wa Ushirika.

"Tuhakikishe kuwa ndani ya Vyama vya Ushirika wakulima wanapata huduma bora kama vile upatikanaji wa pembejeo kwa bei nafuu na kwa wakati, elimu ya Ushirika, bima ya afya, masoko na bei nzuri za mazao," alisisitiza Mrajis

Mrajis ameeleza kuwa dhana ya Ushirika ndio njia ya kuinua Uchumi wa watu wengi kwa pamoja hivyo ni muhimu kuzingatia utendaji wenye kuzingatia maadili na taratibu za Ushirika ili kulinda uendelevu wa Vyama na kujenga uchumi imara wa wananchi wanyonge.

Dkt. Ndiege amevitaka Vyama vyote vya Ushirika ambavyo vimepata hati chafu kwa mujibu wa Shirika la Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika (COASCO) kufanya jitihada mahususi za kuondokana na dosari zilizosababisha hati hizo chafu. Alibainisha baadhi ya sababu za hati hizo ni kukosa elimu ya uandishi wa vitabu, utunzaji mbovu wa kumbukumbu na mengine.



*Baadhi ya wajumbe wa Mkutano Mkuu wa 20 Wanachama wa Iringa Farmers Cooperative Union (IFCU)*

# NAIBU MRAJIS AHIMIZA UADILIFU KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA



*Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa 31 wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Kagera – KCU (1990) LTD uliofanyika tarehe 28/04/2021 mjini Bukoba.*

Naibu Mrajis wa Vyama vya Ushirika, Collins Nyakunga, amewataka wanchama wa Vyama vya Ushirika nchini kutekeleza takwa la Kisheria kwa kuchagua Wajumbe wa Bodi watakaowaongoza kwa kipindi cha miaka mitatu (3), kuwachagua Viongozi kwa kuzingatia sifa walizonazo, waadilifu wenye maono na uwezo wa kuongoza kwa kutanguliza maslahi mapana ya wanaushirika.

Naibu Mrajis alikuwa akiongea kwenye Mkutano Mkuu wa 31 wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Kagera – KCU (1990) LTD uliofanyika tarehe 28/04/2021 mjini Bukoba na kuhudhuriwa na Wajumbe kutoka Vyama vya Msingi 135 wanachama wa KCU katika wilaya za Bukoba, Muleba na Misenyi.

Aidha, Naibu Mrajis amevitaka Vyama vya Ushirika nchini kuwa na Mpango Mkakati ili kuwa na Dira ya kutekeleza mipango mbalimbali ya chama na kufanya kuwepo na mwendelezo wa kazi hizo kupitia viongozi watakaochaguliwa kwa nyakati tofauti.

**"Wanaushirika Kuweni makini katika kusimamia chama chenu kwa kuchagua viongozi waadilifu, wenye hofu ya Mungu na wenye maono na wanaopenda kuleta maendeleo kwa wanachama wote; msichague viongozi watakaowapa rushwa,"** amesisitiza Bwana Nyakunga.

Akifungua Mkutano huo, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Brigedia Jenerali Michael Gaguti, katika hotuba iliyosomwa kwaniaba yake na aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Misenyi, Kanali Denis Mwila amewataka wajumbe wa Mkutano Mkuu, kutambua wanalo jukumu kubwa la kubadili maisha ya wakulima kupitia Vyama vyao vya Ushirika.

"Tuhakikishe kuwa wakulima wetu wanahudumiwa ipasavyo ili waweze kuwa na imani na Chama chenu cha KCU. Nitoe wito pia muendelee kushirikiana na Halmashauri zetu pamoja na kituo chetu cha utafiti cha TACRI Maruku katika kuwapatia wakulima mbinu za kilimo bora cha kisasa," alisema Mkuu wa Mkoa wa Kagera.

Katika kkutano huo, Mkuu wa Mkoa alisisitiza Kabla ya kuanza msimu mpya wa 2021/22, Chama kinatakiwa kuweka mipango madhubuti itakayopunguza kero kwa wakulima hususani kupata fedha za kuwalipa ndani ya muda mfupi baada ya kupima kahawa zao kwenye AMCOS na Chama Kikuu cha Ushirika kinatakiwa kusafirisha Kahawa kwa haraka kutoka kwenye Vyama vya msingi ili kupunguza muda wa malipo kwa wakulima.

"Mnatakiwa kuchakata/kukoboa kahawa zenu haraka ili kuwahi masoko kwani kumbukumbu zinaonesha kuwa masoko ya mwanzo yanakuwa na bei ya kuridhisha. Aidha, mnatakiwa kuwasimamia wakulima wenu waliopo kwenye AMCOS ili wazalishe kahawa kwa mujibu wa Sheria ya zao la Kahawa ikiwa ni pamoja na kuvuna kahawa iliyokomaa na kuikausha kwa kiwango kinachotakiwa," amesisitiza Mkuu wa Mkoa wa Kagera.

Mkuu wa Mkoa wa Kagera aliipongeza Bodi ya KCU na Watendaji kwa kufanikiwa kurejesha mikopo takriban Shilingi 18 bilioni za msimu huu 2020/21. Pamoja na pongezi amewaasa kwamba jukumu la usimamizi wa mikopo ni endelevu, hivyo waendelee kusimamia fedha na mali nyingine za ushirika kwa kutanguliza maslahi mapana na Wanachama.

## WAKULIMA WA MVOMERO WAANZA KUNUFAIKA NA ONGEZEKO LA BEI YA KOKOA KUPITIA MFUMO WA STAKABADHI ZA GHALA

Mfumo wa Stakabadhi za Ghala umeendelea kuwa mkombozi wa mkulima kutokana na ongezeko la bei linalotokana na ukusanyaji na uuzaji wa pamoja unaozingatia ubora. Mfumo huu umekuwa ukitumika katika maza o ya Korosho, Kahawa, kakao, Ufuta, Choroko, Dengu, Mbaazi na Soya. Mkoani Morogoro, mfumo wa Stakabadhi za Ghala haukuwahi kutumika katika zao lolote kabla, licha ya kwamba mkoa huu unzalisha mazao yanayoweza kuhifadhika na kuuzwa kwa kupitia mfumo huu.

Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa kushirikiana na Bodi ya Stakabadhi za Ghala (WRRB) na Soko la Bidhaa (TMX) walifanya uhamasishaji wa matumizi ya mfumo katika zao la Kakao Wilaya ya Mvomero kwa kutoa elimu kwa wakulima kupitia Vyama vya Ushirika. Wilaya hii inakadiriwa kuzalisha kilo laki moja (100,000) za Kakao kwa mwaka

kutoka katika Kata za Kweuma, Diongoya, Mhonda na sungaji katika Tarafa ya Turiani.

Wakulima wa Kata hizo waliamua kwa pamoja kutekeleza na kuanza matumizi ya mfumo ambapo kupitia mnada wa kwanza uliofanyika mapema mwezi wa saba mwaka 2021 wakulima walinufaika na ongezeko la bei baada ya kupokea jumla ya Tsh 21,173,040 ikiwa ni mauzo ya Kakao. Kiasi hiki cha fedha kimepatikana baada ya kuuza kilo 5,040 kwa bei ya Tsh 4,201 kwa kilo tofauti na Tsh 3,500 waliyokuwa wakilipwa kabla ya kuanza matumizi ya mfumo wa Stakabadhi za Ghala.

Manada huu uliendeshwa na Soko la Bidhaa Tanzania (TMX) ukishuhudiwa na wakulima waliojitokeza katika Kata ya Mhonda ambapo ndiyo kituo cha makusanyo ya Kakao Kiwilaya.

Kabla ya matumuzi ya mfumo huu, wakulima wamekuwa wakizalisha Kakao bila kuwa na uhakika wa kupata mnunuzi hivyo kupelelekea kutokuwa na nguvu ya upangaji bei ambapo bei ya Kakao iliyokaushwa mara moja iliuzwa kwa Tsh 2,300 hadi 2,500 wakati Kakao iliyokaushwa vizuri ilikuwa Tsh 3,500 hadi 3700.

Mnada wa pili ulifanyika tarehe 14 Agosti 2021 ambapo zilipokelewa kilo elfu kumi na mbili (12,000) kutoka kwa wakulima wa Wilaya ya Mvomero na Wilaya ya Kilombero ambao wamehamasika kutumia mfumo huu. Ni matarajio yetu kuwa wakulima wengi wataendelea kukusanya mazao yao katika Vyama vyao vya Msingi ili yaweze kupelekwa katika ghala kuu kwa ajili yaminada.



*Viongozi wa AMCOS za Mhonda na Kweuma wakishuhudia upokeaji wa Kakao katika Ghala la Mhonda*

# STAKABADHI ZA GHALA KUENDELEA KUMPAISHA MKULIMA

**Kuna msemo wa miaka mingi usemao kilimo ni uti wa mgongo. Kilimo ambacho kinazalisha mazao mbalimbali ikiwemo mazao mbalimbali yanayozalishwa na kuuzwa kwa kutumika mfumo wa Stakabadhi ya Ghala. Mfumo wenye malengo ya kumpatia mkulima faida kutokana na mauzo yanayofanyika kupitia bei za ushindani kupitia minada.**

Katika kutekeleza Mfumo huu wa Stakabadhi za Ghala, Serikali kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) na Soko la Bidhaa Tanzania (TMX) imekuwa ikihimiza matumizi ya Mfumo kwenye mauzo ya mazao ya Choroko, Soya, Ufuta, Mbaazi na Dengu kwa lengo la kuhamasisha uzalishaji wenye tija na kupata bei zenye ushindani.

Katika mahojiano ya makala hii Mrajis Msaidizi wa Mkoa wa Ruvuma Bumi Masuba anaeleza Mfumo wa Stakabadhi za Ghala ulianza mkoani hapo katika msimu wa Korosho wa 2016/17 na kuanza Mfumo huu kwa mazao ya jamii ya mikunde kuanzia 2018/19 kwa Wilaya za Ruvuma kwa elimu ya Mfumo wa Stakabadhi ya Ghala.

"Kimsingi Mfumo huu tulianza kwanza kutoa elimu kwa wakulima kuhusu uuzaji na ununuzi wa mazao kupitia Stakabadhi za Ghala kupitia Vyama vya Ushirika ili wakulima waelewe watakavyonufaika na Mfumo huo.

**"Mfumo unawezesha wakulima kuwa pamoja kukutana na wanunuzi na kuwa na nguvu ya pamoja katika kupanga bei zenye tija akifafanua kuwa zao la Ufuta kabla ya mfumo bei ilikuwa kati ya Shillingi 800-1000 na bei baada ya mfumo iliongezeka hadi kufikia Sh.1, 800 - 3,143, Soya kabla ya mfumo iliuzwa kwa Sh. 250-500 baada ya mfumo imeuzwa Sh. 640 – 1,526, Mbaazi kabla ya mfumo iliuzwa kwa Sh.150- 200 bei baada ya mfumo Sh. 400-880, Korosho kabla ya mfumo Sh.1,200-2,000 bei baada ya mfumo 2,200- 3,700" anaeleza Mrajis**

Akizungumzia mwenendo wa bei za minada ya Ufuta, Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika Tunduru (TAMCU) Musa Manjaule alieleza kuwa bei za mauzo ya Ufuta kupitia minada ambayo tayari imefanyika siku za karibuni za msimu wa mwaka 2020/21 zimekuwa zikiongezeka hivyo kuwapa wakulima tija na bei zenye ushindani.

Mwenyekiti huyo alibainisha kuwa katika Mnada wa kwanza wa Ufuta Wilayani Tunduru uliofanyika Nguvumali AMCOS Kijiji cha Lukumbule Kata ya Lukumbule mzigo wa Ufuta uliuzwa wa Kilo 634,915 uliuzwa kwa Shillingi

2,204. Wakati mnada wa pili wa Ufuta uliofanyika Mtiti AMCOS Kijiji cha Morandi Kata ya Marumba kiasi cha Kilo 251,348 cha Ufuta uliuzwa kwa Shillingi 2,220 na mnada wa tatu ulifanyika Mruji AMCOS Kijiji cha Mchesi Ufuta Kilo 429,947 ulizwa kwa wastani wa bei ya Sh.2, 280. Kutokana na ongezeko hilo la bei kupitia minada hiyo Mwenyekiti alisema Mfumo huo unakubalika sana na wakulima Wilayani Tunduru na kuwataka wakulima kuendelea kutumia nguvu ya pamoja katika kupanga bei unaompa urahisi mnunuzi kupata mzigo mwingi wa uhakika kwa urahisi na kumpunguzia gharama za uendeshaji.

Aidha, katika maeneo mengi mfumo huu umekuwa mkombozi kwa wakulima kwani utekelezaji wake huzingatia makusanyo ya mazao ya wakulima katika maghala kuanzia katika Vyama vya Ushirika na baadae kufikishwa katika maghala makuu ya Ushirika, jambo ambalo hutoa fursa ya ukaguzi wa mazao hayo ili kuhakikisha ubora wa mazao kabla ya kuuzwa unazingatiwa. Baadhi ya masuala ya muhimu yanayoangaliwa kwa umakini wakati wa kukusanya mazao kuanzia ngazi ya Vyama vya Msingi ni pamoja na Uzito wa mzigo, usafi, unyevu na vifungashio sahihi kwaajili ya usalama na usafirishaji wa mazao.

Agnes Mchoka mkulima kutoka Lukumbule AMCOS Wilayani Tunduru amesema Mfumo wa Stakabadhi Ghalani umewapa uhakika wa usalama wa wakulima na familia zao kutokana na mfumo huo kutumia malipo kwa njia ya Benki. Mkulima huyo alifafanua kuwa kabla ya matumizi ya mfumo wakulima walikuwa wakipata adha ya wizi na ujambazi pindi wanapouza mazao yao na kupokea malipo mkononi jambo ambalo alisisitiza kuwa lilikuwa likihatarisha usalama wao. Akiongeza kuwa malipo kwa njia ya benki pia yameondosha uwezekano wa mkulima kupokea hela pungufu au pengine hela ambazo zinakuwa na dosari nyingine.

# HALI YA UKUSANYAJI NA UUZAJI WA MAZAO YA KOROSHO NA UFUTA MKOANI LINDI KWA MSIMU 2020/2021

**Mkoa wa Lindi ni mojawapo kati mikoa inayolima mazao ya Korosho na ufuta nchini ambapo mazao haya hukusanywa na kuuzwa kupitia Vyama Vikuu vya Ushirika vya RUNALI (Ruangwa, Nachingwea na Liwali) na Lindi Mwambao (Lindi Vijijini (Mtama), Kilwa na Lindi Manispaa). Kilimo cha mazao hayo kimekuwa ndio uti wa mgongo wa uchumi wa wananchi wa Mkoa huo.**

Kwa Upande wa RUNALI, msimu 2020/2021 chama kilikusanya na kuuza jumla ya Tani 44,382 za korosho zenye thamani ya Shilingi za Kitanzania Billioni mia moja na nne milioni kumi na mbili mia tano tisini na moja elfu mia moja themanini na nne tu (Tsh 104,012,591,184) na jumla ya Tani 34,742 za ufuta. Kwa Upande wa Chama Kikuu cha Ushirika Lindi Mwambao, msimu 2020/2021 cha kilikusanya jumla ya Tani 21,021 za Korosho ambazo ziliuzwa kwa jumla ya Shilingi za Kitanzania Bilioni arobani na nane milioni mia sita sabini na tisa mia tisa themanini na tano elfu mia sita thelethini na tisa tu (Tsh.48,679,985,639) na jumla ya Tani 27,541 zenye thamani ya Shilingi za Kitanzania Bilioni Arobaini na tisa milioni mia tatu thelathini na tisa mia tano thelathini na nne elfu mia saba sitini na tatu tu (Tsh. 49,339,534,763) Katika kuhakikisha kuwa wakulima wanapata tija kwenye kwenye kilimo cha mazao hayo, Vyama Vikuu vya RUNALI na Lindi Mwambao kwa kushirikia na Wataalam wa Halmashauri zote za mkoa wa Lindi wanahamasisha wakulima kusafisha mashamba yao na kutumia pembejeo kwa usahihi kwa ushauri unaotolewa na Maafisa Ugani. Kwa msimu 2020/2021 Vyama hivi viliweka mkakati wa kuhakikisha kuwa pembejeo za zao la Korosho zinapatikana kwa wakati na kwa bei nafuu ambapo Makampuni mbalimbali yakubali kuvikopesha Vyama hivi pembejeo kwa masharti nafuu kwa mfano Salfa ya unga ilisambazwa kwenye vyama kwa bei ya Shilingi 30,000 na kukopeshwa kwa wakulima kwa bei ya Shilingi 32,000.

Mfumo unaotumika kukusanya mazao ya Korosho na Ufuta ni mfumo wa Stakabadhi za ghala ambapo kwa upande vya Vyama Vikuu ya RUNALI na Lindi Mwambao wanawalipa wakulima moja kwa moja baada ya fedha kuingizwa kwenye akaunti ya mauzo (Collection account). Kwa mujibu wa maelezo ya baadhi ya wakulima na Viongozi wa Wilaya inaelezwa kuwa mfumo huu wa kuwalipa wakulima moja kwa moja kutoka wenye akaunti kuu ya mauzo umekuwa ni wa haraka na nafuu kwa wakulima na umeondoa changamoto nyingi zilizotokana na wakulima kutokulipwa fedha zao kwa wakati. Mfumo uliokuwa unatumika awali ulileta changamoto mbalimbali zilizotokana na fedha nyingi za wakulima kupotelea kwenye vyama vya msingi kutokana na vyama hivyo kuwa na watu ambao hawana uwezo wa kusimamia na kulipa fedha za wakulima matokeo yake kutumia fedha hizo kwa ajili ya kulipa gharama nyingine za uendeshaji pasipo kujua kuwa fedha hizo ni za wakulima waliouza mazao yao.

Kwa msimu wa 2020/2021 Vyama hivi vimepata mafanikio mbalimbali ikiwa ni pamoja na;

- Kuongezeka kwa uelewa wa wakulima kuhusu mfumo wa stakabadhi za ghala unaotumika kukusanya mazao yao.
- Wakulima kuwa na mwamko chanya wa kufungua akaunti za benki ili malipo ya mazao yao yaweze kulipwa kupitia akaunti hizo
- Kutumia mfumo wa kulipa moja kwa moja kutoka akaunti ya makusanyo ya malipo kumesaidia wakulima kupata fedha zao kwa wakati mara tu baada ya minada kufanyika
- Kupata pembejeo kwa wakati jambo linalopelekea kuongezeka tija kwa mkulima
- Kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao kutokana na hatua ya baadhi ya wakulima - kutumia kanuni za kilimo bora
- Vyama kuwa na akaunti maalum kwa ajili ya kukusanyia fedha za mbembejeo

Licha ya mafanikio hayo, bado vyama Vikuu vya RUNALI na Lindi Mwambao vinapitia changamoto mbalimbali kama vile;

- Kukosekana kwa uaminifu na uadilifu hasa wakati wa ukusanyaji na usafirishaji wa mazao ya mkulima. Baadhi ya wakulima wamekuwa wakilipwa pesa pungufu kutokana na baadhi ya viongozi na wasafirishaji kuwaibia wakulima mazao yao hasa wakati wa kusafirisha kutoka ghala la chama cha msingi kwenda ghala kuu kwa mfano Tathmini iliyofanywa Sehemu ya Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika Visivyo vya Kifedha ilibaini kuwa jumla ya korosho zenye uzito wa **Kilo 78,500** zilizosafirishwa kutoka vyama vya Likowele AMCOS, Tumiliki AMCOS na Umoja AMCOS kwenda kwenye ghala kuu la UMOJA AMCOS zilikuwa na upungufu wa jumla ya **Kilo 1,539.**
- Wakulima kuchelewa kurejesha mikopo ya pembejeo wanazokopeshwa
- Uelewa mdogo wa baadhi ya wakulima kuhusu mifumo ya kibenki jambo linalosababisha kuchelewa kulipwa fedha zao kutokana na kushindwa kutoa taarifa sahihi za akauti zao za benki hivyo kusababisha fedha zao kurejeshwa "rejection"
- Vifungashio kwa ajili ya mazao ya korosho na ufuta haviwafikii wakulima kwa wakati



# USHIRIKA KUJALI JAMII KWA VITENDO




*Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Siku ya Ushirika Duniani (wa kwanza kushoto) akifuatiwa na mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Ushirika Bi. Theresia Chitumbi pamoja na wanakamati wa maandalizi ya Siku ya Ushirika Duniani 2021 wakikabidhi mahitaji katika Kituo cha Afya cha Maili Tano, mkoani Tabora.*

Ushirika umetajwa kuwa nyenzo muhimu katika kuijali jamii na kuleta ushirikiano mzuri baina ya watu katika Jamii kwa malengo ya kuhakikisha jamii inauwa na mahusiano mema kwaajili ya kudumisha na ustawi wa Jamii na hatimaye kuleta matokeo chanya kiuchumi.

Hayo yamesemwa na Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Ushirika Bi. Theresia Chitumbi Julai 01, 2021 wakati akikabidhi mahitaji mbalimbali ya kibinadamu katika Kituo cha Afya Maili Tano Halmashauri ya Manispaa ya Tabora akiwa ameambatana na kamati ya maandalizi ya Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani mkoani Tabora.

Mwenyekiti Bi. Theresia ameeleza kuwa kujali Jamii ni miongoni mwa Misingi ya Kimataifa ya Ushirika ambapo kamati hiyo imetumia fursa ya maadhimisho ya Siku ya Ushirika ambayo imezinduliwa rasmi Juni 29, 2021 na kilele kufikiwa Julai, 03, 2021 kutekeleza msingi huo wa kujali Jamii. Kamati hiyo imekabidhi mahitaji ya kibinadamu mbalimbali yakiwemo Sabuni, Sukari, mafuta, miswaki, dawa za miswaki, taulo za kike vyenye thamani ya Shilling Millioni Mbili.

“Vyama vya Ushirika ni vina majukumu mengi ikiwemo Kujali Jamii kwani Ushirika unaundwa na Jamii hivyo

kuleta mahitaji haya katika Kituo hiki cha Afya Maili Tano ni sehemu ya kutimiza wajibu na msingi wa Ushirika tumeona ni vyema kutekeleza hili hasa tunapoelekea kilele cha maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani," alisema Bi. Theresia

Kamati ikikabidhi mahitaji hayo Mwenyekiti wa Kamati ya maandalizi ya Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani Dkt. Gervas Machimu nae alieleza kuwa sambamba na makabidhiano hayo maadhimisho yanaendelea katika Viwanja vya Nanenane Ipuli mkoani Tabora. Akaongeza kuwa Kituo hicho cha Afya ni jirani na eneo la Uwanja hivyo kamati imetekeleza wajibu huo kwa kuzingatia jamii iliyopo jirani na eneo la Maadhimisho hayo.

Dkt. Machimu alitoa mwaliko kwa wananchi kutembelea mabanda ya maonesho ambapo wadau wengi wa Sekta ya Ushirika kutoka maeneo mbalimbali wameshiriki pamoja na shughuli nyingine zinazofanyika uwanjani hapo ikiwa ni pamoja na semina, makongamano, upimaji wa afya, ushauri wa masuala ya Kilimo, huduma za kisheria na huduma nyingine nyingi.

Akipokea mahitaji hayo kwa niaba ya Kituo hicho muuguzi Zaituni Ally ameishukuru kamati hiyo ya Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani na kupongeza hatua iliyochukuliwa kwani mahitaji hayo yanakwenda kusaidia kuongeza utoaji wa huduma bora kwa wagonjwa wanaofika katika kituo hicho.

Katika hatua nyingine Kamati hiyo iliendelea na makabidhiano ya mahitaji ya kibinadamu katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Kitete mkoani Tabora ambapo Mwenyekiti wa Shirikisho Theresia Chitumbi pamoja na Kamati ya maandalizi walikabidhi mahitaji mbalimbali yakiwemo sabuni, mafuta, Sukari, miswaki, dawa za miswaki, taulo za kike vyenye thamani ya Shillingi Millioni moja na nusu.

Akipokea mahitaji hayo Mganga Mfawidhi wa Kituo hicho Dkt. Mark Waziri aliishukuru Kamati ya Maandalizi kwa niaba ya wanaushirika na kutoa wito kwa wadau wa Ushirika kuendelea kushirikiana na Jamii katika kuboresha na kuendeleza huduma bora za Jamii zinazonguka maeneo yenye Shughuli za Ushirika kwani kufanya hivyo kunakuza uhusiano mwema na hatimaye kuongeza tija ya uchumi wa Jamii na Taifa.




*Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Ushirika Bi. Theresia Chitumbi akiwa ameambatana na Kamati ya maandalizi ya Siku ya Maadhimisho ya Siku ya Ushirika, mkoani Tabora*

# MCHANGO WA VYAMA VYA USHIRIKA WA NYUMBA KUFIKIA AZMA YA NYUMBA KWA WOTE NA UKUAJI WA MIJI

**Ndugu Msomaji wa Jarida la Ushirika**, Katika toleo lililopita tuliaangalia mchango wa vyama vya ushirika wa nyumba kufikia azma ya nyumba kwa wote na ukuaji wa miji. Katika toleo hilo tuliangazia zaidi maana ya vyama vya ushirika wa nyumba, vyama vya ushirika wa nyumba katika nchi mbalimbali na hapa nchini Tanzania na hatimaye tukagusia kidogo umuhimu wa vyama vya Ushirika wa nyumba katika mnyororo wa thamani wa nyumba.

Katika toleo hili, tunaendelea kuangalia umuhimu wa vyama vya ushirika wa nyumba katika mnyororo wa thamani wa nyumba.

**Ndugu Msomaji wa Jarida la Ushirika**, kabla ya kuendelea zaidi ninaomba tufahamu kwamba vyama vya ushirika wa nyumba hapa nchini vimetambuliwa katika sera mbalimbali ambazo ni pamoja na Sera ya Maendeleo ya Ushirika (2002) na Sera ya maendeleo ya makazi ya mwaka 2000, japokuwa bado havijapewa msukumo mkubwa ili kuwezesha wananchi wengi wa kipato cha chini kujiunga ili kupata makazi bora kwa bei nafuu. Ndiyo maana utaona kwamba idadi ya vyama hivi bado ni vichache sana. Takwimu zinaonesha kwamba hadi kufikia Mwezi Oktoba, 2018 idadi ya vyama vya ushirika wa nyumba nchini vilikuwa ni 16 tu. Mkoa wa Dar es Salaam ukiwa unaongoza kwa kuwa na vyama sita (6) ikifuatiwa na Mikoa ya Kagera na Mwanza ambavyo vilikuwa na vyama (2). Mikoa mingine ilikuwa na chama kimoja ikiwemo; Arusha, Dodoma, Tanga, Iringa na Mtwara.

# UMUHIMU WA VYAMA VYA USHIRIKA WA NYUMBA KATIKA MNYORORO WA THAMANI WA NYUMBA

**Ndugu Msomaji wa Jardia la Ushirika**, muhimu wa vyama vya ushirika wa nyumba unajionyesha katika shughuli zake kwenye mnyororo wa thamani wa nyumba yaani ***Housing Delivery Value Chain*** katika hatua saba (7) ambazo ni:- upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya makazi, umilikishaji, miundombinu mikubwa ya kufungua miji,

ujenzi,Uuzaji na uhamishaji milki, Matunzo na uhifadhi wa nyumba na Huduma za miundombinu ya kijamii na kiuchumi.

Umuhimu wa ushirika wa nyumba katika kila hatua ya mnyororo wa thamani wa nyumba umeelezwa katika kielelezo kinachofuta hapa chini.



## Upatikanaji wa Ardhi

Chama cha Ushirika wa Nyumba kinabeba dhamana ya upatikanaji wa ardhi kwa wanachama wake ambapo wanachama huweza kulipa kidogo kidogo. Husaidia wanachama kupata viwanja katika kwa urahisi katika makazi rasmi. Hivyo husaidia katika upangaji wa Miji.

## Umilikishaji

Vyama uhakikisha kuwa wanachama wake wanamilikishwa ardhi.

## Miundombinu mikubwa ya kufungua mitaa

Huwezesha miundombinu mikubwa kujengwa kutokana na wingi wa wakazi.Wakati mwingine chama huchangia gharama za miundo mbinu mikubwa kutoka na uwezo na wingi wa wanachama.

## Ujenzi

Gharama za ujenzi hubebwa kwa njia mbalimbali hususan mikopo kutoka katika taasisi za fedha.Wanachama hupata unafuu wa gharama za ujenzi kutokana na wingi wa nyumba zinazojengwa kwa wakati mmoja na wakati mwingine katika eneo moja.

## Uuzaji na Uhamishaji Milki

Wanachama wanaweza kupata mikopo au kwakudhaminiwa na chama kununua nyumba ambazo zimekamilika.

## Matunzo na Uhifadhi wa nyumba

Chama kinakuwa na mfuko wa utunzaji na matengenezo ya nyumba ambapo mwanachama atakuwa anachangia kwenye chama chakena pale ambapo ukarabati utatakiwa,baada ya kupata kibali cha kufanya ukarabati kutoka kwenye mamlaka husika mfuko huo utaweza kutumika kwa utaratibu ambao utakuwa umewekwa. Hivyo kupitia ushirika nyumba huweza kutunzwa vizuri wakati wote.

## Huduma za miundombinu ya kijamii na kiuchumi

Huduma za miundombinu za kijamii na kiuchumi kama vile mfumo wa maji, maji taka, uhifadhi wa taka ngumu.Kugharamiwa kwa pamoja na hivyo hupunguza gharama kwa mwanachama kwa sababu humilikiwa na chama.

# USHIRIKA WA NYUMBA NA MALENGO YA MAENDELEO ENDELEVU

Kwa kutambua umuhimu wa vyama vya ushirika wa nyumba katika mnyororo wa thamani wa nyumba, shirikisho la vyama vya ushirika duniani, limetoa kipaumbele kikubwa katika kufikia malengo ya maendeleo endelevu ya Umoja wa Mataifa (SDGs) ifikapo 2030.

Shirikisho la Vyama vya ushirika Duniani (ICA) linamini kuwa ushirika wa nyumba una jukumu kubwa katika kupunguza umaskini, kuwezesha jitihada za kufikia usawa na usalama katika umiliki wa nyumba. Hivyo tunaangalia azma ya "***Nyumba kwa Wote kwa ukuaji bora wa miji***" tunapaswa kutafakari kwa kina tukirejea katika lengo la 11 la Malengo ya Maendeleo Endelevu. Lengo hilo linakadiria kuwa kufikia mwaka 2030, kutakuwa na upatikanaji wa nyumba za kutosha kwa wote, nyumba salama na zenye gharama nafuu na zenye huduma za kimsingi na zenye kuboresha makazi duni.

Kama ambavyo tumeona kuwa vyama vya ushirika wa nyumba ni nyenzo muhimu katika mnyororo mzima wa upatikanaji wa nyumba. Hivyo, vyama vya ushirika wa nyumba vinapaswa kupewa msukumo mkubwa na kuwekewa mipango madhubuti inayohusisha wadau mbalimbali.

Mwandishi wa Makala hii ni Bwana Bahati J. Rukiko, Afisa Programu Mwandamizi kutoka Taasisi ya Elimu Endelevu ya Ushirika ya Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, Ofisi ya Dodoma. Simu: +255 764 021 915.

# TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA TANZANIA (TCDC)

## NAMBA ZA SIMU ZA TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA TANZANIA (TCDC)




**Maulizo na ushauri:**

Piga *0735 032 348, 0735 032 349*

au

**Piga simu bure(Toll-Free)**

*0800110105, 0800110109*

www.ushirika.go.tz   ushirika@ushirika.go.tz   ushirika_tcdc

@ushirika_tcdc   Tume ya maendeleo ya ushirika

*Limetolewa na*
**Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC)**
Mtaa wa Kuu, S. L. P. 201, **DODOMA.**
Simu: +255 26 23 22456, Telefax: +255 26 23 21973
B.Pepe: **ushirika@ushirika.go.tz** Tovuti: **www.ushirika.go.tz**